

END OF TERM 1 EXAMS

KISWAHILI

FORM ONE

TIME: 1 ½ HOURS

NAME.....ADM NO:.....

SIGN..... INDEX NO:.....

UFAHAMU: (ALAMA 15)

Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo.

Gogo

Umezuka moto kweli, misitu yateketea,
Wachanji wameduwili, hakuna pa kukimbia,
Zimewakwama akili, mashoka yanaungua,
Gogo linawaka moto, wachanji tahadharini.

Kwa kweli kila mahali, halaiki yaumia,
Si Kenya si Shelisheli, mamia yaangamia,
Shikeni yangu kauli, msije kujijutia,
Gogo linawaka moto, wachanji tahadharini.

Ijapokuwa kalili, muda wa kuhadithia,
Yapimeni kwa ratili, haya ninayowambia,
Sijegeuka shubili, tamu mnayodhania,
Gogo linawaka moto, wachanji tahadharini.

Moto huno ni kukuli, hauchomi kuchagua,
Hauna jaji wakili, kwamba utajitetea,
Huchoma kiwiliwili, pingiti likasalia,
Gogo linawaka moto, wachanji tahadharini.

FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657

We mchanji kaa tuli, boresha yako tabia,
Kugwenya lile na hili, magongo kujsombea,
Twaja tujipige wali, siku ya kukufukia,
Gogo linawaka moto, wachanji tahadharini.

Ili wepuke muhali, usije kujililia,
Gogo ulo na kibali, chanja ulilozowea,
Usiyachanje mawili, zani utajibwagia,
Gogo linawaka moto, wachanji tahadharini.

Maswali:

1. Shari hili ni la aina gani? (ala 2)

2. Eleza vina vya shairi hili. (ala 2)

3. (a) Eleza maana ya mizani? (ala 1)

(b) Shairi hili lina mizani ngapi katika ubeti wa tatu mshororo wa kwanza?
(ala 1)

4. Taja kibwagizo cha shairi hili . (ala 1)

5. Taja nchi mbili zilizotajwa katika shairi. (ala 1)

6. Mshairi ametumia uhuru wa kishairi. Eleza huku ukitolea mifano kila maelezo. (ala 4)

7. Eleza maana ya msamiati ufuatao: (ala 1)
- Pingiti –

- Zani –

8. Eleza ujumbe unaowasilishwa na mshairi. (ala 1)

SARUFI: ALAMA 25

1. Pambanua sauti hizi kama ni ghuna au sikhuna. (ala 1)
/s/

/z/

2. Eleza maana ya shadda. (ala 1)

3. Tia shadda kwenye maneno yafuatayo ili kuleta maana iliyo katika mabano.
Ala (kifaa)
Ala (mshangao)
Barabara (njia kuu)
Barabara (sawasawa) (ala 2)

4. Toa mifano miwili ya aina za kamusi. (ala 1)

5. Tunga sentensi moja ili kutofautisha maana ya maneno yafuatayo pafu and bafu. (ala 1)

6. Taja vipashio vya lugha. (ala 2)

7. Andika maneno yenye miundo ya silabi ifuatayo;
KKKI
II (ala 1)
8. Bainisha maneno katika sentensi zifuatazo.
Kitabu kimeanguka chini ya meza. (ala 2)
9. Taja na ueleze aina mbili za viambishi. (ala 2)
10. Jaza viambishi vinavyofaa katika nafasi.
i) Mitikiti ____liyopandwa juzi ____ mimea. (ala 1)
11. Ainisha viambishi katika sentensi ifuatayo:
Walitupongeza. (ala 3)
12. Taja sifa mbili za lugha. (ala 2)
13. Onyesha matumizi ya alama zifuatazo za uafikishaji. (ala 2)
Mshazari –
Koloni –
14. Yaweke maneno yafuatayo katika ngeli mwafaka: (ala 2)
a) Sukari –
b) Chuma –
15. Onyesha matumizi mawili ya kiimbo. (ala 2)

FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657

ISIMU JAMII: (ALAMA 10)

I. Eleza kaida za lugha.

(ala 4)

II. Taja sifa za sajili ya shuleni.

(ala 6)

Kila la Heri.

FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657